SHULE YA SEKONDARI MKALALA,
S.L.P 2,
MUFINDI.
Barua pepe……
Mob. 0769 002 366/0768 360 728.
Tarehe……

Kumb. Na. ……..
Jina la mwanafunzi……..
S.L.P ……
……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MKALALA WILAYA YA MUFINDI, MKOA WA IRINGA MWAKA 2021.

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **kwanza** katika shule ya **Sekondari Mkalala** mwaka 2021. Shule ya sekondari Mkalala ipo katika kata ya Mninga wilaya ya Mufindi Mkoa wa Iringa.

Muhula wa kwanza wa kuanza masomo unaanza tarehe 04/01/2019 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 11/01/2021 ndani ya siku saba (7).

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia.

2.1 **SARE YA SHULE.**

A. Wasichana

i. Shati mbili (2) rangi nyeupe mikono mirefu.
ii. Sketi moja (1) light blue.
iii. Sketi moja (1) nyeusi.
iv. Soksi nyeupe.
v. Viatu jozi mbili (2) rangi nyeusi vya kufunga na kamba visivyo na kisigino kirefu.

NB. Sketi ziwe ndefu zinazopita magoti.

vi. Sweta rangi ya blue.
vii. Sare ya michezo ni tracksuit za bluu zenye mistari rangi nyeupe na raba nyeupe.
viii. Sweta rangi ya blue.
ix. Vifaa vya usafi kama ndoo ya lita 10 na mfagio

B. Wavulana.

a) Shati mbili (2) rangi nyeupe mikono mirefu.
b) Suruali moja (1) rangi nyeusi isiwe ya kubana.
c) Suruali moja (1) rangi ya light blue isiwe ya kubana.
d) Viatu jozi mbili (2) rangi nyeusi vya kufunga na kamba visivyo na kisigino.
e) Soksi nyeusi.
f. Sweta rangi ya blue.
g. Sare ya michezo ni tracksuit za bluu zenye mistari rangi nyeupe na raba nyeupe.
h. Vifaa vya usafi kama vile ndoo ya lita 10 na mfagio
i. Fail kubwa 1 (Boxfail)

2.2 Daftari kubwa (counter-book), kalamu na mkebe wa hesabu.

2.3 Chakula cha wanafunzi wa kutwa, nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu.

2.4 Mahitaji muhimu ya kibinadamu.

3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote ya wizara ya elimu, sayansi, teknologia na ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya waziri Mkuu-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa mavazi ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule muda wote.
i) Kutunza mali za umma.

3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

a) Wizi.
b) Uasherati.
c) Ubakaji.
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, coceine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba.
i) Kuoa au kuolewa.
j) Kutoa mimba.
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) Kuwa na simu ya mkononi.

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.

a) Medical Examination form ambayo itajazwa na mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hiyo itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

MKUU WA SHULE

FOMU YA TAARIFA YA MWANAFUNZI

Jina lilioandikishwa……..
Tarehe ya kuzaliwa……..
Mahali alipozaliwa: Kijiji…….Kata…….
Tarafa…….Wilaya…….
Jina la Baba……Yu hai/amefariki……
Jina la Mama……..Yu hai/amefariki……
Mama ana watoto wangapi……..wakike……wakiume…….
Wewe ni mtoto wa ngapi kwa mama…….
Makazi yako kwa sasa: kijiji…….Kata…….
Tarafa …….Wilaya ……
Anwani ……
Jina la atakayegharamia mahitaji shuleni ……
Uhusiano wake kwako…….
Kazi yake……
Anwani yake…….
Shule uliyotoka ……
Kidato ulichopokelewa kujiunga……..
Kukiwa na tatizo taarifa ipelekwe kwa……
Anwani yake……
Uhusiano wenu……..
Sahihi ya mwanafunzi……tarehe……

MKATABA WA MWANAFUNZI

Mimi……nakubali kupokea nafasi niliyopewa katika shule hii ya kibao Sekondari.
Naahidi kuwa nitahudhuria shule na vipindi vyote ndani na nje kama inavyohitajika,nitatii sharia na kanuni za shule kwa nidhamu na uaminifu wa hali ya juu,nitashirikiana na wanafunzi wenzangu , walimu, wazazi na jamii kuinua taaluma na kudumisha elimu bora.
Vitendo vyote viovu ndani na nje ya shule kwangu ni mwiko.
Jina……sahihi……tarehe……

TAMKO LA MZAZI

Mimi……..ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi……. Nakiri kusoma na kuyaelewa maagizo, sheria na kanuni za shule na kukubali mwanangu ajiunge na shule ya sekondari Mkalala. Naahidi kuwa nitatumia uwezo wangu wote kumpa/kumgharamia mahitaji yote yanayotakiwa kwa muda mwafaka ili kumjengea mazingira mazuri ya kupata Elimu bora.

Natambua kuwa kutogharamia mahitaji na kutotoa ushirikiano katika kufuatilia mwenendo na maendeleo ya mwanangu ni kukiuka wajibu wangu. Sipo tayari kuwa sababu ya usumbufu na maendeleo duni ya mwanangu.

Jina……..Sahihi……..tarehe……

MEDICAL EXAMINATION FORM

MKALALA SECONDARY SCHOOL,
P. O. BOX 02,
MUFINDI.

DATE…….....

THE MEDICAL OFFICER,

……..

RE: MEDICAL EXAMINATION IN RESPECT OF…….

I would be very grateful if you would kindly examine the above named student as his/her fitness for admission to school as a day secondary school Education under the item listed below:

……..
Head of school

Examine and certify the following items

1. EARS……..
2. EYES……..
3. BLOOD COUNT……
4. S. T. D…….
5. SPLEEN…….
6. CHEST……..
7. TYPHOID……
8. STOOL…….
9. URINE……..
10. T. B……
11. PREGNANCE (TO GIRLS ONLY)…….
12. Any physical/mental defects or impairment identified……..
13. Any additional comments……

I have examined the above named student and certify his/her fit/unfit for admission to pursue secondary

…… ……

MEDICAL OFFICER'S SIGN & STAMP DATE